**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**636** **TEHAMA**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2018**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A**, na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka katika Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Fafanua kwa kifupi mambo manne yanayoweza kuhatarisha usalama wa wanafunzi na vifaa vya kujifunzia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la TEHAMA.
2. Eleza kwa kifupi mambo manne muhimu ya kuzingatia katika utunzi wa maswali ya kuchagua jibu sahihi katika somo la TEHAMA.
3. Bainisha vifaa vinne na namna vinavyoweza kutumika kufundishia mada ya kuelezea kwa usahihi habari iliyosemwa.
4. Toa tofauti nne kati ya magazeti na majarida.
5. Ainisha vifaa vinne anavyohitaji mwalimu wa somo la TEHAMA katika kuandaa azimio la kazi.
6. Bainisha matatizo manne yanayowakumba wakutubi katika kazi yao ndani ya Maktaba.
7. Changanua tofauti nne kati ya barua ya kawaida na barua ya rejesta.
8. Pendekeza mbinu nne zinazoweza kutumika kufundishia mada ya usikivu kwa wanafunzi wa somo la TEHAMA.
9. Fafanua kwa ufupi aina kuu nne za upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi katika somo la TEHAMA.
10. Bainisha njia nne zinazoweza kumsaidia mwalimu wa somo la TEHAMA kupata zana za kufundishia na kujifunzia.

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **Manne** katika sehemu hii.

11. Jadili mambo matano yanayoweza kuonesha ubaguzi wa kijinsia wakati wa ufundishaji na ujifunzaji somo la TEHAMA.
12. Eleza kwa kina mambo matano yanayoweza kuathiri uwasilishaji wa habari iliyosemwa.
13. Tathmini mchango wa mtandao wa intaneti katika kuleta msawazo wa mawasiliano katika jamii.
14. Toa mifano na kufafanua nyanja zozote tano za utambuzi kwa mujibu wa mtaalamu Benjamin Bloom zinavyotumika katika upimaji wa maendeleo ya wanafunzi.
15. Jadili mambo matano yanayoweza kumfanya mwanafunzi akose usikivu darasani.
16. Chambua misingi mitano anayotakiwa kuzingatia mwalimu wa somo la TEHAMA katika kubuni na kutengeneza zana.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org